ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***No. 11*** ***2nd December, 2022***

***ACT SUPPLEMENT***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 45 Vol. 103 Dated 2th December, 2022*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

# SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI, 2022
## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Malengo ya Sheria.
5. Misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi.

SEHEMU YA PILI
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

6. Uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.
7. Majukumu ya Tume.
8. Uanzishwaji wa Bodi.
9. Majukumu ya Bodi.
10. Kamati za Bodi.
11. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.
12. Muda wa kuhudumu wa Mkurugenzi Mkuu.
13. Watumishi wa Tume.

SEHEMU YA TATU
USAJILI WA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI

14. Usajili wa wakusanyaji na wachakataji.
15. Rejesta ya wakusanyaji na wachakataji.
16. Kipindi cha usajili.

17. Ukaguzi wa taarifa zilizosajiliwa.
18. Kufutwa kwa usajili.
19. Makosa yanayohusiana na usajili.
20. Rufaa kuhusiana na usajili.
21. Usajili wa taasisi za umma.

SEHEMU YA NNE
UKUSANYAJI, UTUMIAJI, UFICHUAJI NA UHIFADHI WA TAARIFA BINAFSI

22. Ukusanyaji wa taarifa binafsi.
23. Chanzo na utoaji wa taarifa binafsi.
24. Usahihi wa taarifa binafsi.
25. Taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.
26. Mipaka ya ufichuaji wa taarifa binafsi.
27. Usalama wa taarifa binafsi.
28. Uhifadhi na utoaji wa taarifa binafsi.
29. Usahihishaji wa taarifa binafsi.
30. Katazo la uchakataji wa taarifa binafsi nyeti.

SEHEMU YA TANO
USAFIRISHAJI WA TAARIFA BINAFSI NJE YA NCHI

31. Kusafirisha taarifa binafsi kwenda nchi yenye ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi.
32. Kusafirisha kwenda nchi isiyo na ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi.

SEHEMU YA SITA
HAKI ZA WAHUSIKA WA TAARIFA

33. Haki ya kupata taarifa binafsi.
34. Haki ya kuzuia uchakataji unaoweza kumuathiri mhusika wa taarifa.
35. Haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni ya utangazaji wa biashara.
36. Haki kuhusiana na uamuzi unaofanywa kiotomatiki.
37. Haki ya fidia.
38. Kurekebisha, kuzuia, kufuta na kuharibu taarifa binafsi.

SEHEMU SABA UCHUNGUZI WA
MALALAMIKO

39. Malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi.
40. Notisi ya uchunguzi.
41. Usiri wa uchunguzi.
42. Mamlaka ya Tume wakati wa uchunguzi.
43. Kuizuia Tume.
44. Kutumia msaada wa mtu au mamlaka nyingine.
45. Notisi ya utekelezaji.
46. Notisi ya adhabu.
47. Faini za kiutawala.
48. Marejeo ya uamuzi.
49. Haki ya rufaa.
50. Malipo ya fidia.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA FEDHA

51. Vyanzo vya fedha za Tume.
52. Usimamizi wa fedha.
53. Makadirio ya mapato na matumizi na udhibiti wa fedha.
54. Matumizi ya fedha.
55. Makadirio ya nyongeza.
56. Akaunti na ukaguzi.
57. Taarifa za kila mwaka na mikataba ya utekelezaji.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI MENGINEYO

58. Mazingira yanayoondolewa katika mawanda ya Sheria hii.
59. Amri ya uhifadhi.
60. Makosa ya ufichuaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria.
61. Makosa ya uharibifu, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria.
62. Makosa yanayotendwa na kampuni au shirika.
63. Adhabu ya jumla.
64. Kanuni.
65. Kanuni za maadili ya ulinzi wa taarifa binafsi.



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 11 YA 2022

NAKUBALI,

SAMIA SULUHU HASSAN
*Rais*
27 Novemba, 2022

Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa lengo la kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi, na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na kuanza kutumika

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar isipokuwa kwa Tanzania Zanzibar haitatumika kwa mambo yasiyo ya muungano.

Tafsiri

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa ulinzi wa taarifa binafsi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na mkusanyaji au mchakataji na kupewa jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

majukumu yaliyoainishwa katika Sheria hii;

"kanuni za maadili" maana yake ni kanuni zinazobainisha maadili na miiko ya wachakataji na wakusanyaji wa taarifa binafsi zinazoandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 65;

"mahakama" maana yake ni mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza suala husika;

"mchakataji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo inachakata taarifa binafsi kwa ajili na kwa niaba ya mkusanyaji chini ya maelekezo ya mkusanyaji, isipokuwa kwa watu ambao, chini ya mamlaka ya moja kwa moja ya mkusanyaji, wanaruhusiwa kuchakata taarifa binafsi, na itajumuisha mwakilishi wake;

"mhusika wa taarifa" maana yake ni mhusika wa taarifa binafsi zinazochakatwa kwa mujibu wa Sheria hii;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 11;

"mkusanyaji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo peke yake au kwa pamoja na taasisi nyingine huamua madhumuni na njia za uchakataji wa taarifa binafsi; na pale ambapo madhumuni na njia za uchakataji zimebainishwa katika sheria,

"mkusanyaji" ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma iliyoteuliwa kwa mujibu wa sheria na itajumuisha mwakilishi wake;

"mpokeaji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi, taasisi ya umma au mtu mwingine yeyote ambaye anapokea taarifa binafsi kutoka kwa mkusanyaji;

"mtaalamu wa afya" maana yake ni mtu anayetoa huduma za afya na kutambuliwa hivyo kwa mujibu wa sheria;

Sura ya 13

"mtoto" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mtoto;

"mtu mwingine" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma tofauti na-

(a) mhusika wa taarifa;
(b) mkusanyaji au mchakataji; na
(c) mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya kuchakata

taarifa binafsi;

"nyaraka" maana yake ni njia yoyote ambayo taarifa imerekodiwa, iwe imechapishwa au ipo kwenye mkanda au filamu au kwa njia ya kielektroniki au vinginevyo na inajumuisha ramani, mchoro, picha, filamu, filamu ndogo, mkanda wa video, rekodi ya sauti au rekodi inayosomeka kwa mashine au rekodi yenye uwezo wa kuzalishwa kutoka kwa rekodi inayosomeka kwa mashine kwa njia ya vifaa au programu, au mchanganyiko wa zote mbili, vinavyotumiwa na mkusanyaji kwa madhumuni ya kutunza kumbukumbu;

"rejesta" maana yake ni rejesta iliyoanzishwa na Tume kwa mujibu wa kifungu cha 15;

"taarifa binafsi" maana yake ni taarifa kuhusu mtu anayetambulika ambazo zimetunzwa kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na-

(a) taarifa binafsi zinazohusu rangi, asili ya kitaifa au kikabila, dini, umri au hali ya ndoa ya mtu binafsi;

(b) taarifa binafsi zinazohusu elimu, historia ya matibabu, jinai au ajira;

(c) namba yoyote ya utambulisho, alama au namna nyingine maalum inayomtambulisha mtu binafsi;

(d) anwani, alama za vidole au kundi la damu la mtu binafsi;

(e) jina la mtu binafsi linaloonekana katika taarifa binafsi za mtu mwingine anayehusiana naye au pale ambapo ufichuzi wa jina hilo utadhihirisha taarifa binafsi za mtu;

(f) taarifa iliyotumwa kwa mkusanyaji wa taarifa binafsi na mtu, ambayo ni wazi kuwa taarifa hiyo ni binafsi au ya siri, na majibu kwa taarifa hiyo yanaweza kufichua maudhui ya taarifa ya awali, na mtazamo au maoni ya mtu mwingine yeyote kuhusu mhusika wa taarifa;

"taarifa binafsi nyeti" inajumuisha-

(a) taarifa ya vinasaba, taarifa inayohusu watoto, taarifa inayohusu makosa, miamala ya kifedha ya mtu binafsi au hatua za kiusalama, taarifa za kibayometriki;



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(b) ikiwa imechakatwa, ni taarifa binafsi inayoonyesha asili ya rangi au kabila, itikadi za kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, ushirika, uanachama wa vyama vya wafanyakazi, jinsia na taarifa za kiafya au mahusiano ya kingono; na

(c) taarifa binafsi yoyote ambayo kwa mujibu wa sheria za nchi inachukuliwa kuwa ina athari kubwa kwa haki na maslahi ya mhusika wa taarifa;

"taarifa za vinasaba" maana yake ni taarifa binafsi yoyote inayotokana na uchambuzi wa tindikali ya vinasaba;

"Tume" maana yake ni Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6;

"uchakataji" maana yake ni uchambuzi wa taarifa binafsi, kwa njia za kiotomatiki au vinginevyo, kama vile kukusanya, kurekodi au kushikilia taarifa binafsi au kufanya uchambuzi kwenye taarifa binafsi, ikiwa ni pamoja na-

(a) kuzipanga upya, kuzichukua na kuzitumia kama zilivyo au kuzibadilisha;

(b) kuzirejesha au kuzitumia; au

(c) kuziwianisha, kuzichanganya, kuzuia matumizi yake, kuzifuta au kuziharibu;

"usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi" maana yake ni usafirishaji wowote wa taarifa binafsi wa kimataifa, unaovuka mipaka kwa njia za kielektroniki au njia nyingine; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mawasiliano.

Malengo ya Sheria

4. Malengo ya Sheria hii ni-

(a) kudhibiti ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi;

(b) kuhakikisha kwamba ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi za mhusika wa taarifa unaongozwa na misingi iliyowekwa katika Sheria hii;

(c) kulinda faragha za watu binafsi;

(d) kuweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi wa kulinda taarifa binafsi; na



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(e) kuwapa wahusika wa taarifa haki na nafuu katika kulinda taarifa binafsi kutokana na ukusanyaji na uchakataji usiofuata masharti ya Sheria hii.

Misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi

5. Mkusanyaji au mchakataji atahakikisha kwamba taarifa binafsi-

(a) zinachakatwa kihalali, kwa haki na kwa uwazi;
(b) zinakusanywa kwa madhumuni mahususi, yaliyobainishwa na halali, na taarifa hizo hazitaendelea kuchakatwa kwa namna tofauti na madhumuni yaliyoainishwa;
(c) zinatosheleza na ni muhimu kwa madhumuni ya uchakataji kama ilivyokusudiwa;
(d) ni sahihi na pale inapobidi, zinaboreshwa kwa kuchukua hatua zote muhimu kuhakikisha taarifa binafsi zisizo sahihi zinafutwa au kurekebishwa bila kuchelewa;
(e) zinahifadhiwa katika namna inayoruhusu utambuzi wa mhusika wa taarifa kwa muda usiozidi ule unaohitajika kwa madhumuni ya uchakataji wa taarifa binafsi husika;
(f) zinachakatwa kwa kuzingatia haki za mhusika wa taarifa;
(g) zinachakatwa kwa namna ambayo itahakikisha usalama wa taarifa binafsi, ikijumuisha ulinzi dhidi ya uchakataji usioruhusiwa au ulio kinyume cha sheria na dhidi ya hasara, uharibifu au madhara yoyote, kwa kutumia hatua sahihi za kiufundi au za kiutawala; na
(h) hazisafirishwi nje ya mipaka ya nchi kinyume cha masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

6.-(1) Inaanzishwa Tume itakayojulikana kama Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

(2) Tume itakuwa taasisi nafsi yenye mamlaka ya urithishaji wa kudumu na lakiri yake, na kwa jina lake

itakuwa na uwezo wa-

(a) kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika, kutoa mali na kuingia mikataba au makubaliano mengine yoyote;

(b) kushtaki au kushtakiwa; na

(c) kutekeleza jukumu lolote lingine ambalo taasisi nafsi yoyote kisheria inaweza kutekeleza kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Majukumu ya Tume

7. Majukumu ya Tume yatakuwa-

(a) kufuatilia utekelezaji wa Sheria hii kwa wakusanyaji na wachakataji;

(b) kusajili wakusanyaji na wachakataji kwa mujibu wa Sheria hii;

(c) kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;

(d) kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;

(e) kutoa elimu kwa umma kwa kadri itakavyofaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;

(f) kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa;

(g) kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyingine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii; na

(h) kutekeleza majukumu mengine ya Tume kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Uanzishwaji wa Bodi

8.-(1) Inaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo itakuwa ni chombo cha usimamizi wa Tume na ambayo itakuwa na wajumbe saba kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti; na

(b) wajumbe wengine watano.

(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watateuliwa



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

na Rais kwa kuzingatia utaratibu kwamba iwapo Mwenyekiti anatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti atatoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.

(3) Wajumbe wengine watano chini ya kifungu kidogo cha (1)(b) watateuliwa na Waziri kutoka miongoni mwa watu wenye sifa na uzoefu katika eneo la TEHAMA, sheria, uhandisi, fedha au utawala.

(4) Ili kudumisha uadilifu wa Tume na kwa madhumuni ya kuepusha mgongano wa maslahi, mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume iwapo kutokana na aina ya madaraka aliyonayo anaweza kuwa na ushawishi kwa Tume.

(5) Mkurugenzi Mkuu wa Tume atakuwa katibu wa Bodi.

(6) Masuala mengine kuhusu Bodi na uendeshaji wa shughuli zake yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

Majukumu ya Bodi

9.-(1) Bodi itasimamia utendaji wa Tume ili kuhakikisha kuwa utendaji huo unazingatia sheria na taratibu zinazosimamia Tume.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Bodi itakuwa na wajibu wa-

(a) kutoa miongozo ya kimkakati na kuunda sera za uendeshaji na usimamizi wa Tume;
(b) kusimamia shughuli na utendaji kazi wa menejimenti ya Tume;
(c) kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali, ikijumuisha kuidhinishwa kwa mpango kazi wa mwaka, bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza;
(d) kuidhinisha mipango ya uwekezaji ya Tume;
(e) kuidhinisha ripoti za utendaji kazi wa Tume;
(f) kuidhinisha kanuni za maadili kwa watumishi wa Tume;
(g) kuidhinisha na kusimamia taratibu za usimamizi wa fedha na kanuni za utumishi wa Tume;
(h) kuidhinisha uondoshaji wa mali za Tume; na
(i) kutekeleza wajibu mwingine wowote kwa kadri



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Tume itakavyoona inafaa kwa ajili ya kutimiza malengo yake kwa mujibu wa Sheria hii.

Kamati za Bodi

10. Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kuunda na kuteua kutoka miongoni mwa wajumbe wake, kamati zozote kadri itakavyoona inafaa.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu

11.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atateuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ana sifa zifuatazo:

(a) amehitimu katika chuo kikuu kinachotambulika na ana angalau shahada ya kwanza katika nyanja za TEHAMA, uhandisi, sheria, uchumi, fedha au utawala;

(b) ana uzoefu wa utumishi usiopungua miaka kumi katika angalau moja ya nyanja zilizotajwa katika aya (a); na

(c) ana ujuzi au utaalamu katika nyanja ya ulinzi wa taarifa.

Muda wa kuhudumu wa Mkurugenzi Mkuu

12. Mkurugenzi Mkuu atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na baada ya kipindi hicho kumalizika, anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

Watumishi wa Tume

13.-(1) Tume, kwa kuzingatia sheria za utumishi wa umma, itaajiri watumishi kwa idadi itakayohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume.

(2) Tume inaweza kuteua washauri na wataalam katika taaluma mbalimbali kwa kuzingatia vigezo na masharti yatakayowekwa na Tume.

## SEHEMU YA TATU
## USAJILI WA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI

Usajili wa wakusanyaji na wachakataji

14.-(1) Mtu hatakusanya au kuchakata taarifa binafsi bila kusajiliwa kama mkusanyaji au mchakataji chini ya Sheria hii.

(2) Mtu anayekusudia kukusanya au kuchakata



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

taarifa atawasilisha maombi ya usajili kwa Tume.

(3) Tume inaweza, katika muda utakaoainishwa katika kanuni, kukubali au kukataa maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2).

(4) Tume itatoa cheti cha usajili kwa mkusanyaji au mchakataji aliyekidhi matakwa ya usajili na kusajiliwa chini ya kifungu hiki.

(5) Endapo Tume itakataa maombi ya usajili itapaswa kumtaarifu mwombaji kwa maandishi juu ya uamuzi wake na sababu ya uamuzi huo.

Rejesta ya wakusanyaji na wachakataji

15.-(1) Tume itaanzisha na kutunza rejesta ya wakusanyaji na wachakataji waliosajiliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Rejesta ya wakusanyaji na wachakataji itajumuisha taarifa kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(3) Mkusanyaji au mchakataji anaweza, wakati wowote, kuomba kwa Tume kuhuisha au kubadili taarifa yoyote iliyoingizwa katika rejesta.

Kipindi cha usajili

16.-(1) Kipindi cha usajili kitakuwa ni miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa kwa cheti cha usajili.

(2) Maombi ya kuhuisha usajili yatawasilishwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya tarehe ya kuisha kwa kipindi cha usajili kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Ukaguzi wa taarifa zilizosajiliwa

17. Kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni na baada ya kulipwa kwa ada iliyoainishwa, Tume inaweza kuruhusu mtu yeyote kupekua na kupakua taarifa yoyote iliyoingizwa katika rejesta.

Kufutwa kwa usajili

18. Tume inaweza kufuta usajili uliofanyika chini ya Sheria hii kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Makosa yanayohusiana na usajili

19. Mtu atakayekiuka masharti ya Sehemu hii au kutoa taarifa za uongo au za kupotosha wakati wa usajili au uhuishaji anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika kifungu cha 63.

Rufaa kuhusiana na

20. Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

usajili

Tume chini ya Sehemu hii anaweza kuwasilisha rufaa kwa njia ya maandishi kwa Waziri.

Usajili wa taasisi za umma

21. Mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, taasisi za umma zinazoshughulika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi zitachukuliwa kuwa zimesajiliwa chini ya Sheria hii na zitapaswa kuzingatia masharti ya Sheria.

## SEHEMU YA NNE
## UKUSANYAJI, UTUMIAJI, UFICHUAJI NA UHIFADHI WA TAARIFA BINAFSI

Ukusanyaji wa taarifa binafsi

22.-(1) Sehemu hii itatumika kwa-

(a) ukusanyaji na uchakataji wowote wa taarifa binafsi uliofanywa kwa taarifa yote au sehemu ya taarifa hiyo kwa njia ya kielektroniki au isiyo ya kielektroniki;

(b) uchakataji wa taarifa binafsi unaofanywa katika utekelezaji wa majukumu ya mkusanyaji anayeishi katika Jamhuri ya Muungano au katika sehemu ambayo sheria za Jamhuri ya Muungano zinatumika kwa mujibu wa sheria za kimataifa;

(c) uchakataji wa taarifa binafsi unaofanywa na mkusanyaji au mchakataji anayeishi nje ya Jamhuri ya Muungano, ikiwa uchakataji huo umefanyika nchini na sio kwa madhumuni ya kupitisha nchini taarifa binafsi kwenda nchi nyingine.

(2) Mkusanyaji atakusanya taarifa binafsi iwapo-

(a) taarifa binafsi inakusanywa kwa madhumuni halali yanayohusiana na kazi ya mkusanyaji; na

(b) ukusanyaji wa taarifa binafsi ni muhimu au unatokana, au kuhusiana moja kwa moja, na madhumuni halali.

(3) Mkusanyaji hatakusanya taarifa binafsi kwa njia zisizo halali.

Chanzo na utoaji wa taarifa binafsi

23.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), mkusanyaji atakusanya taarifa binafsi moja kwa moja kutoka kwa mhusika wa taarifa.

(2) Kabla ya kukusanya taarifa binafsi, mkusanyaji atahakikisha kuwa mhusika-



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(a) anatambua madhumuni ya ukusanyaji wa taarifa binafsi;

(b) anafahamu kuwa ukusanyaji wa taarifa binafsi ni kwa madhumuni yaliyoidhinishwa; na

(c) anawafahamu wapokeaji wa taarifa binafsi waliokusudiwa.

(3) Mkusanyaji hatalazimika kuzingatia kifungu kidogo cha (1) iwapo-

(a) taarifa binafsi husika zimekwisha wekwa wazi;

(b) mhusika wa taarifa binafsi ameidhinisha taarifa zake kukusanywa kutoka kwa mtu mwingine;

(c) utekelezaji wake umeshindikana katika mazingira husika;

(d) kutokutekelezwa kwake ni kwa mujibu wa sheria; na

(e) utekelezaji wake unaweza kuathiri madhumuni ya ukusanyaji.

Usahihi wa taarifa binafsi

24. Kwa kuzingatia madhumuni ambayo taarifa binafsi zinapendekezwa kutumika, mkusanyaji ambaye ana taarifa binafsi hatatumia taarifa hizo kwa mazingira yaliyopo bila kuchukua hatua zinazohakikisha kuwa taarifa hizo zimekamilika, ziko sahihi, zinaendana na maudhui na hazipotoshi.

Taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa

25.-(1) Taarifa binafsi zilizokusanywa kwa mujibu wa Sheria hii zitatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

(2) Endapo mkusanyaji ana taarifa binafsi ambazo amekusanya kwa madhumuni maalum, anaweza kutumia taarifa hizo kwa madhumuni mengine iwapo-

(a) mhusika ameidhinisha matumizi ya taarifa binafsi kwa dhumuni hilo;

(b) matumizi ya taarifa binafsi kwa dhumuni hilo yameidhinishwa au kuhitajika kisheria;

(c) dhumuni ambalo taarifa binafsi imetumika linahusiana moja kwa moja na dhumuni la ukusanyaji wa taarifa hiyo;

(d) taarifa binafsi inatumika-

(i) kwa namna ambayo mhusika hatambuliki; au

(ii) kwa madhumuni ya takwimu au utafiti na

haitachapishwa kwa namna ambayo inaweza kumtambulisha mhusika;

(e) mkusanyaji anaamini kwa sababu za msingi kuwa matumizi ya taarifa binafsi kwa hayo madhumuni mengine ni muhimu ili kuzuia au kupunguza madhara kwa uhai au afya ya mtu husika au mtu mwingine, au kwa afya au usalama wa jamii; au

(f) matumizi ya taarifa binafsi kwa hayo madhumuni mengine ni muhimu katika uzingatiwaji wa sheria.

Mipaka ya ufichuaji wa taarifa binafsi

26. Endapo mkusanyaji ana taarifa binafsi, hatafichua taarifa hizo kwa mtu tofauti na mhusika wa taarifa, isipokuwa kwa mazingira yaliyoainishwa katika kifungu cha 25.

Usalama wa taarifa binafsi

27.-(1) Mkusanyaji na wawakilishi wake watahakikisha kuwa taarifa binafsi zinalindwa, kwa kuchukua hatua za kiusalama zinazohitajika kwa usalama wa taarifa hizo dhidi ya upotevu wa kizembe au uteketezaji, ubadilishaji, upatikanaji au uchakataji wa taarifa binafsi bila idhini.

(2) Hatua za kiusalama zitakazochukuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) zinapaswa kuhakikisha kiwango cha usalama kinachohitajika kwa kuzingatia-

(a) mabadiliko ya kiteknolojia na gharama za kutekeleza hatua hizo; na

(b) aina ya taarifa binafsi inayopaswa kulindwa na madhara yanayoweza kutokea kwa mhusika wa taarifa.

(3) Mkusanyaji au mchakataji atapaswa kuteua afisa ulinzi wa taarifa binafsi atakayehakikisha hatua za kiudhibiti na za kiusalama zinachukuliwa ili kulinda taarifa binafsi zinazokusanywa au kuchakatwa.

(4) Utekelezaji wa shughuli za mchakataji utasimamiwa kwa mkataba utakaoainisha uhusiano kati ya mchakataji na mkusanyaji kwa namna ambayo mchakataji atatekeleza shughuli zake kwa maelekezo ya mkusanyaji,



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

na kwamba pamoja na hayo, mchakataji atakuwa na wajibu wa kuhakikisha anazingatia viwango vya usalama sawa na vinavyoelekezwa na Sheria hii.

(5) Mkusanyaji atakuwa na wajibu wa kuitaarifu Tume, haraka iwezekanavyo, kuhusu uvunjifu wa usalama unaoathiri taarifa binafsi zinazochakatwa kwa niaba ya mkusanyaji.

Uhifadhi na utoaji wa taarifa binafsi

28.-(1) Endapo mkusanyaji atatumia taarifa binafsi kwa madhumuni maalum kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25, atatakiwa kuhifadhi taarifa hizo kwa kipindi kilichoainishwa katika sheria zilizopo au kwa kipindi ambacho kitaainishwa katika kanuni ili kuhakikisha kuwa mhusika wa taarifa anapata fursa ya kuzipata taarifa hizo pale atakapozihitaji.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza, kwa kanuni, kuanisha taratibu za uhifadhi na uteketezaji wa taarifa binafsi alizonazo mkusanyaji kwa kuzingatia madhumuni ya uhifadhi.

Usahihishaji wa taarifa binafsi

29.-(1) Endapo katika nyaraka au jalada ambalo upatikanaji wake umeruhusiwa chini ya Sheria hii kuna taarifa binafsi ambazo mhusika wa taarifa hizo anadai kuwa-

(a) hazijakamilika, sio sahihi au zinapotosha; au
(b) haziendani na dhumuni la uhifadhi wa taarifa husika,

mkusanyaji, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, na baada ya kupokea maombi ya mhusika wa taarifa na kujiridhisha nayo, anaweza kurekebisha taarifa hizo.

(2) Mkusanyaji, wakati wa kufanya marekebisho kwenye taarifa binafsi chini ya kifungu hiki, atahakikisha kuwa hafuti kumbukumbu ya maandishi ya nyaraka kama ilivyokuwa kabla ya marekebisho.

(3) Endapo mkusanyaji hataridhika na sababu za maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), anaweza kukataa kufanya marekebisho yoyote kwenye taarifa binafsi na kumtaarifu mwombaji sababu za kukataa maombi.

PARLIAMENT OF TANZANIA • BUNGE LA TANZANIA •

Katazo la uchakataji wa taarifa binafsi nyeti

30.-(1) Mtu hatachakata taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya maandishi ya mhusika wa taarifa.

(2) Ridhaa chini ya kifungu kidogo cha (1) inaweza kuondolewa na mhusika wa taarifa wakati wowote na bila maelezo au gharama yoyote.

(3) Waziri, kupitia kanuni, anaweza kuamua mazingira ambayo katazo la uchakataji wa taarifa binafsi lililoelezwa chini ya kifungu hiki halitaweza kuondelewa hata kwa ridhaa ya mhusika wa taarifa.

(4) Endapo mhusika wa taarifa ambaye ridhaa yake inaombwa kwa madhumuni ya Sheria hii ni mtoto, mtu asiyekuwa na akili timamu au mtu mwingine yeyote asiye na uwezo wa kutoa ridhaa, ridhaa ya mtu huyo itapatikana kutoka kwa mzazi, mlezi, mrithi, wakili wake au mtu mwingine yeyote anayetambulika kisheria kwa niaba yake anayepaswa kutoa ridhaa.

(5) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika iwapo-

(a) uchakataji ni muhimu kwa uzingatiaji wa sheria nyingine;

(b) uchakataji ni muhimu kulinda maslahi muhimu ya mhusika wa taarifa au ya mtu mwingine, iwapo mhusika wa taarifa hawezi kutoa ridhaa yake au hajawakilishwa na mwakilishi wake kisheria;

(c) uchakataji ni muhimu kwa ajili ya kufungua, uendeshaji au utetezi wa madai ya kisheria;

(d) uchakataji unahusiana na taarifa binafsi zilizowekwa wazi kwa umma na mhusika wa taarifa;

(e) uchakataji ni muhimu kwa madhumuni ya tafiti ya kisayansi na Tume, kwa miongozo maalum, imeainisha mazingira ambayo uchakataji huo unaweza kufanyika; au

(f) uchakataji ni muhimu kwa madhumuni ya kitabibu kwa maslahi ya mhusika wa taarifa, na taarifa binafsi nyeti zinazohusika, zinachakatwa chini ya usimamizi wa mtaalamu wa afya kwa mujibu wa sheria inayosimamia huduma hizo.

SEHEMU YA TANO



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

USAFIRISHAJI WA TAARIFA BINAFSI NJE YA NCHI

Kusafirisha taarifa binafsi kwenda nchi yenye ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi

31.-(1) Tume inaweza, kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kuzuia usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi.

(2) Taarifa binafsi itasafirishwa kwenda nchi yenye mfumo wa kisheria unaotoa ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi pale ambapo-

(a) mpokeaji atabainisha kuwa taarifa binafsi ni muhimu kwa utekelezaji wa jukumu lenye maslahi ya umma au kwa mujibu wa shughuli halali za mkusanyaji wa taarifa binafsi; au

(b) mpokeaji atabainisha umuhimu wa kusafirisha taarifa na hakuna sababu ya kudhani kwamba maslahi halali ya mhusika wa taarifa yanaweza kuathiriwa na usafirishaji au uchakataji katika nchi inayopokea.

(3) Mkusanyaji atapaswa, bila kujali kifungu kidogo cha (2), kufanya tathmini ya awali ya umuhimu wa usafirishaji wa taarifa binafsi.

(4) Mpokeaji atahakikisha kuwa umuhimu wa usafirishaji wa taarifa binafsi unaweza kuthibitishwa baadaye.

(5) Mkusanyaji atahakikisha kwamba mpokeaji anachakata taarifa binafsi kwa madhumuni ambayo yalipelekea kusafirishwa kwa taarifa husika pekee.

Kusafirisha kwenda nchi isiyo na ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi

32.-(1) Taarifa binafsi zitasafirishwa kwenda nchi nyingine tofauti na zile zilizotajwa katika kifungu cha 31, ikiwa ulinzi wa kutosha umehakikishwa katika nchi ya mpokeaji na taarifa inasafirishwa kwa dhumuni la kuruhusu uchakataji ulioruhusiwa kufanyika na mkusanyaji.

(2) Utoshelevu wa kiwango cha ulinzi unaotolewa na nchi nyingine utatathminiwa kwa kuzingatia-

(a) mazingira yote yanayozunguka usafirishaji wa taarifa binafsi husika;

(b) aina ya taarifa binafsi;

(c) madhumuni na muda wa uchakataji unaopendekezwa;

(d) nchi ya mpokeaji;

(e) sheria husika zinazotumika katika nchi nyingine; na

(f) kanuni za kitaaluma na hatua za kiusalama ambazo zinazingatiwa katika nchi ya mpokeaji.

(3) Waziri baada ya kushauriana na Tume na kwa kupitia kanuni, ataainisha aina ya uchakataji na mazingira ambayo usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi hautaruhusiwa.

(4) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3), usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda kwa mpokeaji nje ya nchi au katika nchi ambayo haina uhakika wa ulinzi wa kutosha unaweza kufanyika pale ambapo-

(a) mhusika wa taarifa ametoa idhini kwa usafirishaji unaopendekezwa;

(b) usafirishaji ni muhimu kwa utekelezaji wa mkataba kati ya mhusika wa taarifa na mkusanyaji au utekelezaji wa hatua za awali za mkataba zilizochukuliwa kwa kujibu ombi la mhusika wa taarifa;

(c) usafirishaji ni muhimu kwa ajili ya kuingia au kutekeleza mkataba ulioingiwa au utakaoingiwa kati ya mkusanyaji na mtu mwingine kwa maslahi ya mhusika wa taarifa;

(d) usafirishaji ni muhimu au unahitajika kisheria kwa maslahi ya umma, au kwa ajili ya ufunguaji, uendeshaji au utetezi wa madai ya kisheria;

(e) usafirishaji ni muhimu kwa ajili ya kulinda maslahi halali ya mhusika wa taarifa; na

(f) usafirishaji unafanywa kwa mujibu wa sheria, unalenga kutoa taarifa kwa umma na unatoa fursa ya mashauriano kwa umma kwa ujumla au kwa mtu yeyote mwenye maslahi halali kuwasilisha maoni yake kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika sheria.

(5) Bila kuathiri masharti ya Sheria hii, Tume inaweza kuidhinisha usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nchi ya mpokeaji au nchi nyingine yoyote ambayo haijaweka ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi katika

sheria zake, ikiwa mkusanyaji ataihakikishia Tume kwamba kuna ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi, uhuru na haki za msingi za mhusika wa taarifa, na utekelezaji wa haki za mhusika wa taarifa, na kwamba ulinzi huo unaweza kutekelezwa kupitia hatua zinazojitosheleza za kisheria, kiusalama na masharti husika ya mkataba.

## SEHEMU YA SITA
## HAKI ZA WAHUSIKA WA TAARIFA

Haki ya kupata taarifa binafsi

33.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, mhusika wa taarifa ana haki ya-

(a) kufahamishwa na mkusanyaji yeyote endapo taarifa binafsi zinachakatwa na mkusanyaji huyo au mkusanyaji mwingine kwa niaba ya mkusanyaji huyo;

(b) kupewa na mkusanyaji maelezo ya-

(i) taarifa binafsi zinazomhusu;

(ii) madhumuni ya uchakataji; na

(iii) wapokeaji au makundi ya wapokeaji waliopewa au wanaoweza kupewa taarifa hizo;

(c) pale ambapo uchakataji wa taarifa binafsi kwa njia ya kiotomatiki kwa madhumuni ya kutathmini masuala yanayomhusu, umetumika au unaweza kutumika kama msingi pekee wa maamuzi yenye athari kubwa kwake, kufahamishwa na mkusanyaji kuhusu sababu zilizotumika kufikia uamuzi huo.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), mkusanyaji hatalazimika kutoa taarifa kwa mhusika wa taarifa endapo taarifa hizo-

(a) siyo sahihi;

(b) zinahusika katika uchunguzi kwa mujibu wa sheria; au

(c) zimezuiliwa kwa amri ya mahakama.

Haki ya kuzuia uchakataji unaoweza kumuathiri mhusika wa taarifa

34.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), mhusika wa taarifa ana haki ya kumtaka mkusanyaji kupitia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, kusitisha au kutoanza uchakataji wa taarifa binafsi yoyote



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

inayomhusu ikiwa uchakataji huo unaweza kusababisha madhara makubwa kwake au kwa mtu mwingine.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakitatumika katika mazingira yaliyoondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii.

Haki ya kuzuia uchakataji wa taarifa binafsi kutumika kwa madhumuni ya utangazaji wa biashara

35.-(1) Mhusika wa taarifa, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni, anaweza kumtaka mkusanyaji kuacha kuchakata taarifa zake binafsi kwa madhumuni ya matangazo ya biashara.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), mhusika wa taarifa anaweza kuingia mkataba na mkusanyaji kwa madhumuni ya kutumia au kuchakata taarifa zake binafsi kwa ajili ya kunufaika kifedha.

(3) Katika kifungu hiki "matangazo ya biashara" yanajumuisha wasilisho, kwa namna yoyote, ya tangazo la kibiashara linaloelekezwa kwa mtu fulani.

Haki kuhusiana na uamuzi unaofanywa kiotomatiki

36.-(1) Mhusika wa taarifa anaweza, kupitia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni, kumtaka mkusanyaji kuhakikisha kwamba uamuzi wowote unaofanywa na mkusanyaji au kwa niaba ya mkusanyaji ambao una athari kubwa kwa mhusika wa taarifa, hautegemei uchakataji kwa njia ya kiotomatiki pekee.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), pale ambapo uamuzi wenye athari kubwa kwa mhusika wa taarifa unategemea uchakataji wa kiotomatiki pekee-

(a) mkusanyaji atalazimika mapema iwezekanavyo kumtaarifu mhusika wa taarifa kwamba uamuzi ulichukuliwa kwa kutegemea uchakataji wa kiotomatiki; na

(b) mhusika wa taarifa anaweza kumtaka mkusanyaji kushughulikia upya uamuzi.

(3) Kifungu hiki hakitatumika ikiwa uamuzi uliofanywa-

(a) ni muhimu kwa ajili ya kuingia au kutekeleza mikataba kati ya mhusika wa taarifa na mkusanyaji;

(b) umeruhusiwa na sheria yoyote;



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(c) ni kutokana na ridhaa iliyotolewa na mhusika wa taarifa.

Haki ya fidia

37.-(1) Mhusika wa taarifa atakayepata madhara kwa sababu za ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii uliofanywa na mkusanyaji au mchakataji atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutoka kwa mkusanyaji au mchakataji kutokana na madhara hayo.

(2) Mhusika wa taarifa ambaye haki zake zimevunjwa kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti yoyote ya Sheria hii atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutoka kwa mkusanyaji au mchakataji ikiwa-

(a) mlalamikaji ndiye mhusika wa taarifa aliyeathiriwa au mwakilishi wa mhusika wa taarifa ikiwa mhusika ni mtoto au mtu asiye na akili timamu;

(b) haki za mhusika wa taarifa zimevunjwa kwa sababu ya ukiukwaji huo; na

(c) athari hizo zinahusiana na uchakataji wa taarifa binafsi kinyume na masharti ya Sheria hii.

(3) Endapo Tume itajiridhisha na maombi ya mhusika wa taarifa-

(a) kwamba amepata madhara kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii uliofanywa na mkusanyaji au mchakataji kuhusiana na taarifa binafsi yoyote, katika mazingira yanayompatia haki ya kulipwa fidia chini ya kifungu hiki; na

(b) kwamba kuna hatari kubwa ya ukiukwaji zaidi kuhusiana na taarifa binafsi husika katika mazingira hayo,

Tume inaweza kuamuru kurekebishwa, kuzuiwa, kufutwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo.

(4) Tume, pale ambapo imetoa amri chini ya kifungu kidogo cha (3) na endapo itaona kuwa ni busara, inaweza kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kuwajulisha wahusika wengine ambao wamepatiwa taarifa binafsi kuhusu marekebisho, zuio, ufutaji au uharibifu wa taarifa hizo.

(5) Katika kuamua endapo ni sahihi kuhitaji



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

taarifa chini ya kifungu kidogo cha (4), Tume itazingatia idadi ya watu ambao watapaswa kuarifiwa.

Kurekebisha, kuzuia, kufuta na kuharibu taarifa binafsi

38.-(1) Pale ambapo Tume itaridhika kwa maombi ya mhusika wa taarifa kuwa taarifa binafsi zinazomhusu mhusika huyo siyo sahihi, Tume inaweza kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kurekebisha, kuzuia, kufuta au kuharibu taarifa hizo.

(2) Kifungu kidogo cha (1) kitatumika hata kama taarifa binafsi ni kumbukumbu sahihi zilizopokelewa na mkusanyaji au mchakataji kutoka kwa mhusika wa taarifa au mtu mwingine.

(3) Pale ambapo taarifa binafsi siyo sahihi, Tume inaweza kumuelekeza mkusanyaji au mchakataji kurekebisha taarifa hizo kwa kadri itakavyoona inafaa.

(4) Pale ambapo taarifa binafsi zinazolalamikiwa zimerekebishwa, zimezuiwa, zimehuishwa, zimefutwa au zimeharibiwa chini ya kifungu hiki, mkusanyaji au mchakataji atatakiwa kuwataarifu wahusika wengine ambao walipatiwa taarifa binafsi husika kuhusu kurekebishwa, kuzuiwa, kuhuishwa, kufutwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo.

## SEHEMU YA SABA
## UCHUNGUZI WA MALALAMIKO

Malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi

39.-(1) Mtu yeyote atakayebaini kuwa mkusanyaji au mchakataji amekiuka misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume.

(2) Pale ambapo Tume imejiridhisha kuwa kuna sababu za msingi za kuchunguza suala chini ya Sheria hii, Tume inaweza kuanzisha uchunguzi wa malalamiko kuhusiana na suala hilo.

(3) Malalamiko yatakayowasilishwa katika kifungu hiki yatachunguzwa na kumalizika ndani ya siku tisini tangu tarehe ya kupokelewa.

(4) Tume inaweza, kwa kuzingatia mazingira ya malalamiko, kuongeza muda ulioainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) kwa kipindi kisichozidi siku tisini.

Notisi ya

40. Kabla ya kuanza uchunguzi wa malalamiko chini

uchunguzi

ya Sheria hii, Tume, katika namna itakayoainishwa katika kanuni, inapaswa kumpa notisi ya uchunguzi mkusanyaji au mchakataji anayehusika na malalamiko na nia ya kufanya uchunguzi katika suala hilo.

Usiri wa uchunguzi

41.-(1) Uchunguzi wa malalamiko chini ya Sheria hii utafanyika kwa siri.

(2) Mkurugenzi Mkuu au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba yake ya kupokea taarifa binafsi zinazohusu uchunguzi wowote chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote, atapaswa kukidhi matakwa yoyote ya kiusalama kwa kuchukua kiapo cha usiri kinachopaswa kuchukuliwa na watu ambao wanatekeleza majukumu kama hayo.

Mamlaka ya Tume wakati wa uchunguzi

42.-(1) Wakati wa kuchunguza malalamiko, Tume itakuwa na mamlaka ya-

(a) kuita na kumtaka mtu kuhudhuria mbele ya Tume;

(b) kupokea na kukubali ushahidi na taarifa nyingine, kwa kiapo au kwa hati ya kiapo au vinginevyo;

(c) kuingia katika jengo lolote linalomilikiwa na mkusanyaji au mchakataji yeyote kwa ajili ya kujiridhisha endapo jengo hilo linakidhi mahitaji ya usalama;

(d) kumhoji mtu yeyote au kuondoka na kifaa chochote chenye taarifa binafsi katika jengo lolote alimoingia kwa mujibu wa aya (c); na

(e) kuchunguza au kupata nakala za, au dondoo kutoka kwenye vitabu, nyaraka au kumbukumbu nyingine zilizopatikana katika jengo alimoingia kwa mujibu wa aya (c) zenye suala lolote linalohusika na uchunguzi.

(2) Wakati wa uchunguzi wa malalamiko chini ya kifungu hiki, mlalamikaji na mkusanyaji au mchakataji anayelalamikiwa anaweza kupewa nafasi ya kufanya mawasilisho kwa Tume.



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(3) Bila kujali sheria nyingine yoyote, Tume inaweza kuchunguza taarifa binafsi iliyorekodiwa katika namna yoyote inayohifadhiwa na mkusanyaji au mchakataji, na katika kufanya hivyo, Tume haitazuiliwa kupata taarifa yoyote.

(4) Nyaraka au andiko lolote litakalotolewa chini ya kifungu hiki na mkusanyaji au mchakataji au mtu mwingine yeyote, litarejeshwa na Tume ndani ya siku kumi za kazi baada ya maombi kuwasilishwa kwa Tume na mkusanyaji au mchakataji au mtu huyo, lakini hakuna chochote katika kifungu kidogo hiki kitakachoizuia Tume kuhitaji nyaraka au andiko hilo kuwasilishwa tena kwa mujibu wa kifungu hiki.

Kuizuia Tume

43. Mtu ambaye, kuhusiana na utekelezaji wa mamlaka iliyotolewa chini ya Sheria hii-

(a) ataizuia au kuikwamisha Tume katika utekelezaji wa mamlaka yake;

(b) atashindwa kutoa msaada au taarifa zilizoombwa na Tume;

(c) atakataa kuiruhusu Tume, inapotekeleza majukumu yake, kuingia katika majengo yoyote au kuondoka na nyaraka au kifaa chochote chenye taarifa binafsi; au

(d) ataipa Tume taarifa yoyote ambayo ni ya uongo au ya kupotosha,

anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Kutumia msaada wa mtu au mamlaka nyingine

44.-(1) Kwa madhumuni ya kukusanya taarifa au kwa uchunguzi wowote chini ya Sheria hii, Tume inaweza kushirikiana au kumtumia mtu au mamlaka nyingine yoyote kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya kuisaidia Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.

(2) Mtu au mamlaka nyingine itakayoshirikishwa au kutumiwa na Tume kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), itakuwa na mamlaka sawa na mamlaka iliyo nayo Tume katika kutekeleza mamlaka ya uchunguzi kwa mujibu wa Sheria hii.



PARLIAMENT OF TANZANIA • BUNGE LA TANZANIA •

Notisi ya utekelezaji

45.-(1) Pale ambapo Tume imeridhika kuwa mtu ameshindwa kuzingatia kifungu chochote cha Sheria hii, Tume inaweza kutoa notisi ya utekelezaji kwa mtu huyo ikimtaka kuchukua hatua za kurekebisha mapungufu ndani ya kipindi kitakachoainishwa katika notisi.

(2) Notisi ya utekelezaji itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) itaainisha kifungu cha Sheria hii ambacho kimekiukwa;

(b) itaainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana au kuondoa tatizo husika;

(c) itabainisha kipindi ambacho hatua husika zitapaswa kutekelezwa ambacho hakitapungua siku ishirini na moja; na

(d) itaeleza haki ya kukata rufaa.

Notisi ya adhabu

46.-(1) Pale ambapo Tume itajiridhisha kuwa mtu ameshindwa au anashindwa kuzingatia notisi ya utekelezaji iliyotolewa chini ya kifungu cha 45, Tume inaweza kutoa notisi ya adhabu inayomtaka mtu kulipa kwa Tume faini ya kiasi kitakachoainishwa kwenye notisi.

(2) Katika kuamua iwapo inaweza kutoa notisi ya adhabu kwa mtu na kuamua kiasi cha adhabu, Tume itapaswa, kadiri itakavyoona muhimu, kuzingatia-

(a) aina na uzito wa ukiukwaji, na muda ambao ukiukwaji huo umekuwa ukiendelea;

(b) endapo ukiukwaji umefanywa kwa nia ovu au uzembe;

(c) hatua yoyote iliyochukuliwa na mkusanyaji au mchakataji ili kupunguza madhara waliyoyapata wahusika wa taarifa zikiwemo hatua za kiufundi na za kiutawala;

(d) ukiukwaji aliowahi kufanya mkusanyaji au mchakataji awali;

(e) kiwango cha ushirikiano alichoonesha kwa Tume kwa lengo la kurekebisha ukiukwaji na kupunguza athari hasi za ukiukwaji zinazoweza kujitokeza;

(f) aina ya taarifa binafsi zilizoathiriwa na ukiukwaji;



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(g) namna ambayo Tume ilifahamu kuhusu ukiukwaji, ikijumuisha endapo mkusanyaji au mchakataji aliifahamisha Tume;
(h) kiwango ambacho mkusanyaji au mchakataji alizingatia notisi za utekelezaji na notisi za adhabu zilizowahi kutolewa awali;
(i) uzingatiaji wa kanuni za maadili au vigezo na masharti ya usajili;
(j) endapo adhabu itakuwa na ufanisi; na
(k) kigezo kingine chochote kinachoweza kutumika kuongeza au kupunguza adhabu, ikiwa ni pamoja na faida za kifedha alizozipata au hasara alizosababisha, moja kwa moja au vinginevyo, kutokana na ukiukwaji huo.

Faini za kiutawala

47. Kiwango cha juu cha adhabu kinachoweza kutolewa na Tume katika notisi ya adhabu kuhusiana na ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii, ni shilingi milioni mia moja.

Marejeo ya uamuzi

48.-(1) Tume baada ya kuombwa au kwa utashi wake yenyewe inaweza kufanya marejeo ya uamuzi na maelekezo yake iliyoyatoa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu hii.

(2) Baada ya kufanya marejeo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) Tume inaweza kutengua, kubadilisha au kusitisha uamuzi au maelekezo yake iliyoyatoa awali.

Haki ya rufaa

49. Mtu ambaye hataridhika na hatua yoyote ya kiutawala itakayochukuliwa na Tume, ikiwa ni pamoja na maelekezo yaliyotolewa katika notisi ya utekelezaji au adhabu iliyotolewa katika notisi ya adhabu, anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu.

Malipo ya fidia

50.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 37, Tume inaweza pamoja na adhabu nyingine zilizotolewa chini ya Sheria hii, kumuamuru mkusanyaji au mchakataji aliyesababisha madhara kwa mhusika wa taarifa kutokana na ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii kulipa fidia kwa mhusika wa taarifa.



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1)-

(a) mkusanyaji anayehusika katika uchakataji wa taarifa binafsi atawajibika kwa madhara yatakayotokana na uchakataji huo; na

(b) mchakataji anayehusika na uchakataji wa taarifa binafsi atawajibika kwa madhara yatakayotokana na uchakataji huo ikiwa-

(i) hajatekeleza wajibu ulioelekezwa mahsusi kwa wachakataji chini ya Sheria hii; au

(ii) ametenda kinyume na maelekezo halali ya mkusanyaji.

(3) Mkusanyaji au mchakataji hatawajibika kwa namna iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (2) ikiwa mkusanyaji au mchakataji huyo atathibitisha kuwa hakuhusika kwa namna yoyote katika tukio lililosababisha madhara.

(4) Katika sehemu hii, "madhara" yanajumuisha upotevu wa fedha na madhara yasiyohusisha upotevu wa fedha.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha za Tume

51. Fedha za Tume zitajumuisha-

(a) kiasi cha fedha ambacho kinaweza kutengwa na Bunge;

(b) fedha zitakazopatikana kutokana na huduma, ushauri au malipo mengine;

(c) fedha zitakazotokana na michango, zawadi au ruzuku;

(d) mikopo; na

(e) mapato mengine yatakayotokana na utendaji wa shughuli za Tume chini ya Sheria hii.

Usimamizi wa fedha

52. Fedha za Tume zitasimamiwa na Bodi kwa mujibu wa sheria za fedha na zitatumika kugharamia matumizi yanayohusiana na utekelezaji wa majukumu ya Tume chini ya Sheria hii



PARLIAMENT OF TANZANIA BUNGE LA TANZANIA

Makadirio ya mapato na matumizi na udhibiti wa fedha

53.-(1) Mkurugenzi Mkuu atapaswa, katika kipindi kisichopungua miezi mitatu kabla ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, kuandaa na kuwasilisha katika Bodi ili kuidhinisha, bajeti inayojumuisha makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume itawasilisha nakala ya bajeti kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Waziri anaweza kuitaka Tume kufanya marekebisho katika bajeti ikiwa kwa maoni yake bajeti haiwakilishi makadirio sahihi na ya kuridhisha ya mapato na matumizi.

Matumizi ya fedha

54. Matumizi hayatafanyika kutoka kwenye fedha za Tume isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya matumizi yaliyoidhinishwa na Bodi chini ya kifungu cha 53(1) kuhusiana na mwaka wa fedha ambao matumizi yaliidhinishwa.

Makadirio ya nyongeza

55.-(1) Bodi inaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha husika, kuandaa na kuwasilisha kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa makadirio yoyote ya nyongeza ya makadirio ya mwaka husika.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi Mkuu anaweza, pale ambapo dharura imetokea katika utekelezaji wa majukumu ya Tume, kufanya matumizi ambayo hayajaidhinishwa na Bodi ambapo Mkurugenzi Mkuu atalazimika, ndani ya miezi mitatu inayofuata, kuomba idhini ya Bodi kwa matumizi hayo.

Akaunti na ukaguzi

56.-(1) Tume itaweka vitabu vya hesabu na kutunza kumbukumbu sahihi za shughuli zake kwa mujibu wa viwango vya uhasibu.

(2) Tume itapaswa, ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, kuandaa ripoti ya utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka huo wa fedha, na nakala moja ya ripoti hiyo pamoja na nakala ya hesabu zilizokaguliwa zitawasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(3) Hesabu za Tume zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwingine aliyesajiliwa kama mkaguzi chini ya Sheria ya Usajili wa Wakaguzi na Wahasibu aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa dhumuni hilo.

Sura ya 286

Taarifa za kila mwaka na mikataba ya utekelezaji

57.-(1) Ndani ya muda wa miezi miwili baada ya kupokea hesabu zilizokaguliwa na taarifa ya mkaguzi wa hesabu, Mkurugenzi Mkuu atapaswa kuwasilisha kwa Waziri taarifa ya mwaka husika ikijumuisha-

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya mkaguzi kwenye akaunti hizo;

(b) taarifa ya utekelezaji wa malengo muhimu na taarifa nyingine yoyote inayohusiana na utekelezaji wa malengo hayo;

(c) taarifa ya uendeshaji wa Tume katika mwaka wa fedha husika; na

(d) taarifa nyingine kama ambavyo Waziri anaweza kuhitaji.

(2) Waziri atawasilisha Bungeni nakala ya taarifa ya mwaka ya Tume ndani ya miezi miwili au katika mkutano wa Bunge unaofuata.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Mazingira yanayoondolewa katika mawanda ya Sheria hii

58.-(1) Hakuna chochote katika kifungu hiki kitakachomuondolea mkusanyaji au mchakataji wajibu wa kuzingatia misingi ya sheria katika ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi na uchukuaji wa hatua muhimu katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa taarifa binafsi alizonazo.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), uchakataji wa taarifa binafsi unaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii ikiwa uchakataji huo-

(a) unafanywa na mhusika wa taarifa katika shughuli zake binafsi;

(b) unafanywa kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote au amri ya mahakama;

(c) unafanyika kwa madhumuni ya ulinzi na usalama wa Taifa na maslahi ya umma;



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

(d) unafanyika kwa madhumuni ya kuzuia au kubaini uhalifu;

(e) unafanyika kwa lengo la kubaini au kuzuia ukwepaji wa kodi;

(f) unafanyika katika ukaguzi wa ubadhirifu wa fedha za umma; au

(g) ni kwa madhumuni ya upekuzi kwa ajili ya uteuzi katika nafasi ya utumishi wa umma.

(3) Waziri anaweza kuanisha mazingira mengine ambayo yanaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii na masharti mengine kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki.

Amri ya uhifadhi

59.-(1) Tume inaweza kuomba amri ya mahakama kwa ajili ya uhifadhi wa haraka wa taarifa binafsi yoyote, ikijumuisha taarifa binafsi zinazopita katika mfumo, endapo kuna sababu za msingi kuwa taarifa hizo zina hatari ya kupotea au kubadilishwa.

(2) Endapo mahakama itajiridhisha, chini ya kifungu kidogo cha (1), kuwa amri inaweza kutolewa chini ya kifungu kidogo hiki, itatoa amri ya uhifadhi inayoainisha kipindi kisichozidi siku tisini ambapo amri hiyo itatekelezwa.

(3) Mahakama inaweza, kwa maombi ya Tume, kuongeza muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa muda ambao mahakama itaona inafaa.

Makosa ya ufichuaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria

60.-(1) Mkusanyaji ambaye, bila sababu za msingi, atafichua taarifa binafsi kwa njia yoyote ambayo haiendani na madhumuni ambayo taarifa hiyo imekusanywa anatenda kosa.

(2) Mchakataji ambae, bila sababu ya msingi, atafichua taarifa binafsi iliyochakatwa na mchakataji bila idhini ya awali ya mkusanyaji anatenda kosa.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (4), mtu ambaye-

(a) atapata taarifa binafsi, au atapata taarifa yoyote inayojumuisha taarifa binafsi, bila idhini ya mkusanyaji au mchakataji ambaye anahifadhi taarifa hiyo; au

(b) atafichua taarifa binafsi kwa mtu mwingine,
anatenda kosa.

(4) Mtu atakayeuza taarifa binafsi ambayo imepatikana kwa ukiukwaji wa kifungu kidogo cha (1) anatenda kosa.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (4), tangazo linaloonesha kwamba taarifa binafsi inauzwa au inaweza kuuzwa itachukuliwa kuwa ni ofa ya kuuza taarifa binafsi.

(6) Mtu atakayebainika kutenda kosa chini ya kifungu hiki atakapotiwa hatiani atawajibika-

(a) ikiwa ni mtu binafsi, kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi au vyote kwa pamoja; na

(b) ikiwa ni kampuni au shirika, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi bilioni tano.

Makosa ya uharibifu, ufutaji, ufichaji au ubadilishaji wa taarifa binafsi kinyume cha sheria

61. Mtu ambaye ataharibu, atafuta, atapotosha, ataficha au kubadilisha taarifa binafsi kinyume cha sheria anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Makosa yanayotendwa na kampuni au shirika

62. Pale ambapo kosa chini ya Sheria hii limetendwa na kampuni au shirika, kampuni au shirika hilo na kila afisa wa shirika ambaye kwa kujua na kwa makusudi anaidhinisha au kuruhusu ukiukaji atawajibika kwa kosa hilo.

Adhabu ya jumla

63.-(1) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria hii, anatenda kosa na pale ambapo hakuna adhabu mahususi iliyoainishwa, atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

(2) Baada ya mtu kutiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, mahakama inaweza kuamuru



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

kukamatwa kwa vifaa vyake vyenye taarifa binafsi vilivyohusika katika kutenda kosa.

Kanuni

64.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila kujali ujumla wa kifungu kidogo cha (1), kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu hiki zinaweza kuainisha-

(a) mazingira ambayo yataondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii;
(b) taratibu za usajili chini ya Sheria hii;
(c) majukumu ya afisa ulinzi wa taarifa kuhusiana na ulinzi wa taarifa binafsi;
(d) majukumu ya mwakilishi wa mkusanyaji wakati wa kufanya kazi za ukusanyaji na uchakataji kwa niaba ya mkusanyaji;
(e) taratibu za utekelezaji wa haki chini ya Sheria hii;
(f) taratibu za uwasilishaji wa malalamiko chini ya Sheria hii;
(g) masharti ya uchakataji wa taarifa binafsi nyeti;
(h) viwango sahihi vinavyohusiana na usalama wa taarifa vinavyopaswa kuzingatiwa na wakusanyaji;
(i) ada mbalimbali kuhusiana na shughuli za utekelezaji wa masharti ya Sheria hii;
(j) taratibu za uhifadhi na uteketezaji wa taarifa binafsi zinazohifadhiwa na wakusanyaji;
(k) aina ya uchakataji na mazingira ambayo usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi hautaruhusiwa;
(l) jambo lolote ambalo ni muhimu au linafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kanuni za maadili ya ulinzi wa taarifa binafsi

65.-(1) Kila mkusanyaji atapaswa kutengeneza kanuni za maadili au sera kwa ajili ya ulinzi wa taarifa binafsi zitakazobainisha maadili na miiko inayopaswa kuzingatiwa wakati wa ukusanyaji au uchakataji wa taarifa



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

binafsi.

(2) Kanuni au sera chini ya kifungu kidogo cha (1) zitawasilishwa kwa Tume kwa ajili ya mapitio na kuidhinishwa.

(3) Wakati wa mapitio wa kanuni au sera za maadili, Tume itajiridhisha, pamoja na mambo mengine, endapo rasimu za kanuni au sera za maadili zilizowasilishwa zimezingatia masharti ya Sheria hii na ya sekta husika na pale itakapoona inafaa, inaweza kutafuta maoni ya wahusika wa taarifa au wawakilishi wao na kushauriana na mkusanyaji husika kwa madhumuni ya kufanya marekebisho muhimu kabla ya kuziidhinisha.

PARLIAMENT OF TANZANIA
UHURU na UMOJA
BUNGE LA TANZANIA

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8(6))*

TARATIBU ZA BODI

Muda wa wajumbe kushika nafasi

1.-(1) Muda wa wajumbe wa Bodi kushika nafasi utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti - miaka minne; na
(b) wajumbe wengine - miaka mitatu.

(2) Kila mjumbe anaweza kuteuliwa tena kwa muhula mmoja zaidi na baada ya muhula huo kuisha, hatastahili kuteuliwa tena.

(3) Mjumbe yeyote anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa notisi ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi na atakoma kuwa mjumbe kuanzia tarehe iliyoainishwa katika notisi au ikiwa hakuna tarehe iliyoainishwa, kuanzia tarehe ya kupokelewa kwa notisi na mamlaka ya uteuzi.

Ukomo wa wajumbe

2. Mjumbe wa Bodi anaweza wakati wowote kukoma kuwa mjumbe kutokana na sababu zifuatazo:

(a) kupoteza uwezo wa kutekeleza majukumu yake kutokana na ugonjwa wa mwili au akili;
(b) tabia mbaya au utovu wa nidhamu kwa namna ambayo italeta au kuwa na uwezekano wa kuleta sifa mbaya kwa Bodi;
(c) kutohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila kutoa taarifa; au
(d) kujiuzulu; na
(e) kifo.

Kutokuhudhuria vikao vya Bodi

3.-(1) Endapo mjumbe yeyote hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila taarifa, Bodi inaweza kuishauri mamlaka ya uteuzi kuhusu suala hilo na mamlaka ya uteuzi inaweza kutengua uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mjumbe mwingine badala yake.

(2) Iwapo mjumbe yeyote kwa sababu ya ugonjwa, udhaifu au kutokuwepo katika Jamhuri ya Muungano hawezi kuhudhuria kikao chochote cha Bodi, Waziri anaweza kuteua mjumbe wa muda badala yake na mjumbe huyo wa muda atakoma kushika wadhifa huo baada ya mjumbe husika kurejea katika nafasi yake.

Shughuli za Bodi kutobatilishwa kwa sababu ya kasoro

4. Shughuli za Bodi hazitakuwa batili kwa sababu ya kasoro yoyote katika uteuzi wa mjumbe yeyote au kwa kigezo kuwa mjumbe yeyote wakati wa uteuzi hakuwa na sifa au hakustahili kuteuliwa.

Vikao vya Bodi

5.-(1) Bodi itakutana kila robo mwaka kwa nyakati na mahali itakapoona inafaa kwa ajili ya shughuli zake.

(2) Mwenyekiti au pale ambapo hayupo, Makamu Mwenyekiti, anaweza kuitisha kikao maalum au kikao cha dharura cha Bodi.

(3) Kikao cha kawaida cha Bodi kitaitishwa na Mwenyekiti na taarifa inayobainisha mahali, tarehe na muda wa kikao itatolewa kwa



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

wajumbe si chini ya siku kumi kabla ya tarehe ya kikao na endapo Mwenyekiti hawezi kuitisha kikao kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine yoyote au hayupo katika Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao hicho.

(4) Bodi inaweza kuendelea na shughuli zake bila kujali kuwa nafasi yoyote ya ujumbe iko wazi.

Mgongano wa maslahi

6.-(1) Pale ambapo mjumbe wa Bodi wakati wowote ana mgongano wa maslahi kuhusiana na-

(a) suala lolote lililo mbele ya Bodi kwa ajili ya kujadiliwa au kuamuliwa;

(b) jambo lolote ambalo Bodi inaweza kutarajia kuwa linaweza kufika mbele yake kwa ajili ya kujadiliwa au kuamuliwa,

mjumbe atafichua mara moja mgongano wa maslahi kwa wajumbe wengine wa Bodi na kuacha kushiriki katika, au kuendelea kuwa sehemu ya, kujadili au kuamua jambo hilo.

(2) Iwapo Bodi itafahamu kwamba mjumbe ana mgongano wa maslahi kuhusiana na jambo lolote lililo mbele ya Bodi, itamuelekeza mjumbe huyo kutoshiriki au kutoendelea kushiriki katika kujadili au kuamua suala hilo.

(3) Mjumbe wa Bodi atachukuliwa kuwa amekiuka masharti ya aya ndogo ya (1) ikiwa-

(a) atashindwa bila sababu za msingi kuweka wazi maslahi yake kama anavyotakiwa; au

(b) kwa kujua atatoa tamko la uongo au la kupotosha ambalo lina athari katika uamuzi,

mtu huyo atakuwa anatenda kosa na atapaswa kujiuzulu katika wadhifa wake.

Mwaliko wa mtaalamu

7. Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote ambaye si mjumbe kushiriki katika mijadala ya Bodi na kutoa utaalam kama Bodi itakavyohitaji, lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi

8. Akidi katika kikao chochote cha Bodi itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi.

Muhtasari wa vikao

9. Muhtasari wa kila kikao cha Bodi utahifadhiwa na kuthibitishwa na Bodi katika kikao kitakachofuata.

Uamuzi wa Bodi

10. Uamuzi wa Bodi katika suala lolote utakuwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliopo na pale ambapo kura hizo zitalingana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu.

Bodi kuendesha taratibu zake

11. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na mamlaka ya kusimamia taratibu zake kuhusiana na vikao na ufanyaji wa shughuli zake.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Malipo ya wajumbe

12. Wajumbe wa Bodi watalipwa ada na posho kama itakavyoamuliwa na mamlaka husika.

Imepitishwa na Bunge leo tarehe 1 Novemba, 2022.

NENELWA J. MWIHAMBI
*Katibu wa Bunge*

PARLIAMENT OF TANZANIA • BUNGE LA TANZANIA •